



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA MUSOMA



Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na.HMM/P.40/VOL.XII/110

Tarehe: 07 Oktoba, 2022

TANGAZO

NAFASI ZA KAZI

LINARUDIWA

Halmashauri ya Manispaa ya Musoma inakaribisha maombi ya kazi kutoka kwa wananchi wenye sifa zinazotakiwa ili kujaza nafasi ifuatazo:-

1. Katibu Muhtasi Daraja III – Nafasi 2

1.1 Sifa za Mwombaji

Awe amehitimu kidato cha IV na kuhudhuria Mafunzo ya Uhazili na kufaulu mtihani wa Hatua ya Tatu. Awe amefaulu somo la Hatimkato ya Kiswahili na Kiingereza maneno **80** kwa dakika moja na awe amepata mafunzo ya Kompyuta kutoka chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali na kupata cheti katika programu za Window, Microsoft Office, Internet, E-mail na Publisher.

1.2 Majukumu ya Kazi

- Kuchapa barua, taarifa na nyaraka za kawaida.
- Kusaidia kupokea wageni na kuwasaili shida zao, na kuwaelekeza sehemu wanapoweza kushughulikiwa.
- Kusaidia kutunza taarifa/kumbukumbu za matukio, miadi, wageni, tarehe za vikao, safari za Mkuu wake na ratiba ya kazi zingine zilizopangwa wakati unaohitajika.
- Kusaidia kutafuta na kumpatia Mkuu wake majadala, nyaraka au kitu chochote kinachohitajika katika shughuli za kazi hapo ofisini.

2. Mhudumu wa Jikoni/Mess Daraja la II (Kitchen/Mess Attendant) - Nafasi - 2

2.1 Sifa za Mwombaji

- ❖ Awe na Umri wa miaka **18 – 40**.
- ❖ Awe na Elimu ya Kidato cha nne

2.2 Majukumu ya Kazi ni pamoja na kuwa:-

- ❖ Kusafisha Vyombi vya kupikia
- ❖ Kusafisha Vyombo vya kulia chakula
- ❖ Kusafisha Meza itumiwayo kwa kulia chakula
- ❖ Kuwatayarishia Wapishi/Kuandaa vifaa vya Mpishi na Mezani
- ❖ Kusafisha maeneo ya kulia chakula na kupikia
- ❖ Kuwasaidia Wasaidizi na Wapishi

2.3 Mshahara

Ngazi ya mshahara ya **TGOS A**

3. Dereva wa Mashua/Vivuko Daraja la II - Nafasi 1

3.1 Sifa za Mwombaji

- ❖ Awe na Umri wa miaka **18 – 40**.
- ❖ Awe na Elimu ya Kidato cha nne
- ❖ Awe na ujuzi wa kuendesha na kutunza Mashua/Kivuko uliothibitishwa na Chuo cha Dar Es Salaam Marine Institute au Chuo kingine chochote kinachotambuliwa na Serikali kwa muda usiopungua miaka miwili; na waliofuzu mafunzo ya miezi sita uokoaji wa maisha majini, kuogelea na kupanga watu na magari kwenye mashua/vivuko

Masharti:

- Waombaji wote wawe na umri usiozidi miaka **45**
- Maombi yaandikwe kwa mkono na kuambatishwa
 - Cheti cha kuzaliwa
 - Maelezo binafsi(**CV**)
 - Nakala za vyeti vya kuhitimu Elimu ya Msingi, kidato cha nne au sita, cheti cha Taaluma.
 - Picha mbili ndogo “Passport Size”, anuani na namba ya simu
 - **Testimonials, provisional results, Result Slip ya Kidato cha IV na VI havitakubaliwa**
 - Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na Mamlaka husika yaani **NECTA** na **NACTE** na taarifa ya ithibati iambatanishwe kwenye maombi.

NB: Maombi yasiyozingatia masharti tajwa hapo juu hayatashughulikiwa.

Namna ya kutuma maombi.

Maombi yatumwe kwa:-

**MKURUGENZI WA MANISPAA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA MUSOMA,
S.L.P. 194,
MUSOMA**

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 24 Oktoba, 2022

Limetolewa na:-

Bosco O. Ndunguru
**MKURUGENZI WA MANISPAA
HALMASHAURI YA MANISPAA
MUSOMA**